SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI KWA WAATHIRIKA
**WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU** 2023

TUME YA KIMATAIFA YA **HAKI ZA BINADAMU**

JESHI LA WOKOVU

# NIMESIKIA VILIO VYAO



## MSAADA WA KITUO CHA MAOMBI

### KITUO CHA MAOMBI | 1

**Maombi ya Kuelewa**

Usafirishaji haramu wa binadamu, unaojulikana vile vile kama utumwa wa kileo, ni biashara isiyo halali ya binadamu kupitia kwa kuwaandikisha, kutoa misaada au kumpata mtu kwa njia ya kulazimisha, au ulaghai kwa kusudi la kazi za kulazimishwa, utumwa wa deni au unyonyaji wa ngono.

#### ULIJUA?

Idadi ya watu wanaokabiliwa na utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu duniani imeongezeka kufikia wastani wa watu milioni 49.6 siku yoyote. Hii maana yake duniani wastani wa:

- Watu milioni 27.6 wanakabiliwa na kazi za kulazimishwa na unyonyaji wa ngono.
- Watu milioni 22 wanakabiliwa na ndoa za kulazimishwa.

**Chanzo:** Makisio duniani ya Utumwa wa kileo: Kazi za kulazimishwa na Ndoa za kulazimishwa, Shirika la Kimataifa la Kazi, Tembea kwa Uhuru, na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji, Geneva, 2022.

**Maandiko:** 'Hata baada ya siku zile nyingi mfalme wa Misri akafa, wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia; kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa.' (Kutoka 2:23)

#### SHUGHULI YA MAOMBI

Chukua mbegu moja ya mchele na uishike mkononi mwako. Fikiria kwamba mbegu hiyo ni mtu mwenye jina, familia na hadithi. Tumia vipengele vifuatavyo kwa maombi kuongoza maombi yako kwa uelewa:

- Omba macho yetu yafunguliwe tuone aina mbalimbali za usafirishaji haramu wa binadamu na utumwa wa kileo.
- Omba tupate kukua katika uelewa wetu wa nini ni utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu.
- Omba kwamba serikali, mashirika, jamii na watu binafsi wataona, watasikia na hawatakaa kimya.

## KITUO CHA MAOMBI | 2

**Maombi kwa ajili ya Uhuru**

Watu wanaokabiliwa na usafirishaji haramu wa binadamu wana simamiwa na wasafirishaji kwa kutumia vitisho na/au matumizi ya nguvu – iwe ni kimwili au kisaikolojia. Wamenyang'anywa uhuru wao kabisa. Wasafirishaji wanatumia nguvu kusimamia kila eneo la maisha yao – utu wao, mahusiano yao, chaguzi zao, matembezi yao – kufikia mahali wale waliokuwa wanapitia maonevu haya ya kukosa haki hakika wanaamini na kujisikia kwamba hawana uwezo au nguvu za kubadilisha hali yao.

**Maandiko:** 'Hata baada ya siku zile nyingi mfalme wa Misri akafa, wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia; kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa.' (Kutoka 2:23)

### SHUGHULI YA MAOMBI

Chukua kipande cha karatasi na mkasi au kwa kutumia mikono yako kata karatasi kama tendo la alama ya kukata minyororo ya kusimamiwa. Tumia, fuata vipengele vya kuongoza maombi yako ya kutaka uhuru:

- Omba kwa ajili ya usalama na uhuru wa wale wanaokabiliwa na usafirishaji haramu wa binadamu nyumbani na duniani.
- Omba kwamba Mungu atakamata mioyo na maisha ya wasafirishaji na kusababisha wasitishe kuhusika kwao na ukosefu huu wa haki, washiriki katika kurejesha haki na uponyaji katika maisha yao.
- Omba kwamba upande wa madai ya utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu ukomeshwe.

---

## KITUO CHA MAOMBI | 3

Utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu una matokeo yenye madhara kwenye hali ya mwili, hisia, saikolojia na hali ya kiroho ya mtu. Wale ambao wamepitia wamestahimili unyanyasaji usiowezekana unaoweza kuwaathiri kikamilifu kwa muda mfupi na kwa muda mrefu. Kila mmoja lazima apitie mshtuko wa kipekee anapofanya kazi ya kujenga upya maisha yake.

Habari njema ni kwamba kuna TUMAINI. Kuna THAMANI ndani ya kila mmoja ambayo haiwezi kuharibika. Bila kujali mtu amefanywa kujiona ameshushwa kiasi gani, thamani ya Mungu kwa mtu haipotei. Mungu aliwathamini watu wake sana kiasi kwamba alimtuma Mwanae Yesu kama sadaka msalabani. Kupitia kwa sadaka hii ya thamani, uponyaji na maisha mapya yanapatikana kwa wote.

**Maandiko:** 'Hata baada ya siku zile nyingi mfalme wa Misri akafa, wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia; kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa.' (Kutoka 2:23)

### SHUGHULI YA MAOMBI

Chukua plasta kama alama ya uponyaji. Tumia vipengele vifuatavyo vya maombi kuongoza maombi yako kwa ajili ya uponyaji. Baada ya kumaliza kuomba , weka plasta kwenye bango jeusi.

- Omba kwa ajili ya uponyaji wa kimwili, kihisia, kisaikolojia na kiroho wa wale ambao wamepitia usafirishaji haramu wa binadamu.
- Omba kwamba waliopitia usafirishaji haramu wapate mahali salama wanapoweza kupata matunzo ya muda mrefu na msaada kamili. Omba wapate misaada wanayohitaji waweze kuomba misaada, hasa wale ambao wamo katika nchi ambazo hawawezi kuongea lugha ya nchi hizo.
- Omba kwa ajili ya familia zilizotenganishwa na wapendwa wao.

## KITUO CHA MAOMBI | 4

**Maombi kwa ajili ya Haki**

Katika Agano la Kale, neno la kiebrania linalomaanisha haki ni 'mishpat'. Mtazamo huu wa Biblia umejengwa juu ya wazo kwamba mambo yanapokuwa yameenda mrama na maono ya msingi ya Mungu ya salama kwa watu wake na uumbaji wake, na kwa sababu ya ukosefu wa haki unaovamia dunia yetu, ndipo hatua za kuweka mambo sawa na kuleta mrejesho kwenye hali unapohitajika. Mishpat/haki ni kuhusu kutaka kuona dunia ambamo watu wote na uumbaji wanatendewa sawa na wanapewa wanachohitaji ili waweze kushamiri. Ni maono ya maisha ya vingi badala ya mapungufu, kukosa mpangilio na kuonewa kunakotokana na kukosa haki.

Usafirishaji haramu wa binadamu na utumwa wa kileo ni ukiukwaji wa haki za binadamu unaosababisha watu hunyonywa, kutumika, kudhalilishwa na kutendewa isivyo haki.

Tumeitwa kuwa wapatanishi wa haki ya Mungu hapa duniani. Kama wapatanishi, tumeitwa kuwa washirika na wenza na watu walioishi na kupitia kutafuta haki ya Mungu ya kuwaona wakitendewa kwa sawa, washamiri na waishi maisha ya vingi.

**Maandiko:** 'Hata baada ya siku zile nyingi mfalme wa Misri akafa, wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia; kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa. Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo. Mungu akawaona wana wa Israeli, na Mungu akawaangalia' (Kutoka 2:23-25)

### SHUGHULI YA MAOMBI

Chukua kalamu uandike ' KOMESHA' kwenye kiungo kwenye mnyororo wa karatasi. Tumia vipengele vifuatavyo vya maombi viongoze maombi yako ya kutafuta haki:

- Omba haki itendeke kwa niaba ya wale wanaokandamizwa kupitia kwa usafirishaji haramu na utumwa wa kileo.
- Omba mnyororo na rushwa vikome.
- Omba kwa ajili ya watu binafsi walio mstari wa mbele wakipambana na ukosefu huu wa haki.

## KITUO CHA MAOMBI | 5

**Maombi kwa ajili ya Kanisa kuinuka**

Jeshila Wokovu kimkakati limejipanga duniani kote kuomba, kuzuia, kulinda, kushiriki, kuwa wenzi na kuhusika na kushitaki, kutengeneza sera na kazi ya uhakika (ushahidi kulingana na utafiti). Hii sio kazi ambayo inaweza kufanywa na mtu mmoja au wawili au hata mashirika machahe. Kila mmoja anahitajika – mapambano ni ya wote. Inuka, Kanisa! Inuka, Jeshi la Wokovu!

**Maandiko:** 'Hata baada ya siku zile nyingi mfalme wa Misri akafa, wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia; kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa. Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo. Mungu akawaona wana wa Israeli, na Mungu akawaangalia' (Kutoka 2:23-25).

### SHUGHULI YA MAOMBI

Tafuta nchi katika ramani ya dunia na omba kwa ajili ya Jeshi la Wokovu na Kanisa liinuke. Andika maombi kwa ajili ya Kanisa katika nchi hiyo kwenye karatasi yenye gundi  na weka karatasi hiyo kwenye nchi kwenye ramani ya dunia. Tumia vipengele vya maombi vifuatavyo viongoze maombi yako ya Kanisa liinuke:

- Omba kwa ajili ya kuwezeshwa kwa kanisa liinuke liwe sehemu ya ufumbuzi wa kukomesha utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu duniani.

- Omba kwa ajili ya ushirikiano wa ushirika kati ya Kanisa kimkakati tusimame tumeungana na tusaidiane tunapofanya kwa pamoja kukomesha utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu.

- Omba kwa ajili ya Kanisa litoe faraja inayoonekana, msaada na ulinzi kwa watu ambao wameishi na kupitia utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu.

**MSAADA WA KITUO CHA MAOMBI ULIOTENGENEZWA NA**

Kapteni Maryellen Walters (Katibu wa Divisheni wa Vijana na Watakaji wa Divisheni ya Hawai na Kisiwa cha Pasifiki)

Meja Ray Lamont (Mratibu wa Teritori wa majibu ya Utumwa wa kileo na Usafirishaji haramu wa Binadamu – Canada na Bermuda; Caribbean na Marekani Kaskazini Mratibu MSHTR wa Kanda; Naibu Mwenyekiti wa Baraza la Kimataifa MSHTR.